# UKWELI KUHUSU

# DA'AWA YA

# SHEIKH

# MUHAMMAD IBN ABDIL WAHAB -RAHIMAHULLAH-

## MAJIBU DHIDI YA UONGO NA UPOTOFU WA KHALIFA KHAMIS

MUANDISHI

AL AKH QASSIM MAFUTA QASSIM

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote na shukrani zote.
Ni zako wewe sifa njema vile zinavyolingana na utukufu wako na ukubwa wako ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike na pale unaporidhika na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu Mtume wetu Muhammad na jamaa zake na maswahaba zake wote na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Mnamo tarehe 22/Shawwaal/1428 H sawa na 02/11/2007 M. Siku ya Ijumaa baada ya swala ya magh'ribi nilipokea kiitachwo ''UPOTOVU WA MADHEHEBU YA WAHABI'' kitabu ambacho mwandishi wake ni Khalifa Khamis Mohammed.

Kitabu hiki kilianza kuchapishwa miaka ishirini iliyopita chapa ya kwanza ni ya Des 1987, lakini Allah akawa amekadiria kuwa miaka yote hiyo pamoja na kuwa niliwahi kukisikia na kukiona lakini sikuweza kukisoma kitabu hicho hadi kufikia siku hiyo niliyoitaja –Qadarullahi wamashaa fa'ala-.

Kitabu hicho nilianza kukisoma siku hiyo hiyo na mpaka kufikia magh'ribi ya siku ya jumapili ya 04/11/07 niliweza kukimaliza kitabu hicho –pamoja na kutingwa na shughuli za usomeshaji- na baada ya hapo niliamua kuwasha Computer na kuanza kuyaandika haya yaliyomo kwenye kitabu hiki huku nikitarajia malipo kutoka kwa Allah pekeyake na kupata msaada wake na tawfiq yake s.w.t.

Lakini jambo kubwa linalonisikitisha mimi ni kimya cha wenye kujua ambao wameuona upotovu uliomo ndani ya kitabu hicho cha Khalifa Khamis kisha wao wakaamua kuunyamazia kimya.

Kwahakika muandishi wa kitabu hicho amedhihirisha chuki zake za wazi dhidi ya da’awa ya haki da’awa ya salaf swalihi mpaka kufikia kumpelekea chuki hizo kumtoa nje ya uadilifu aliouamrisha Allah s.w.t. katika Qur’an pale aliposema;

"ياأيها الذين آمنوا كونوا قوّامين لله شهدآءَ بالقسطِ ولا يَجرمنّكم شَنَآن قومٍ ألاّ تعدلوا اعدلوا هو أقرب للتقوى..".

‘‘Enyi ambao wameamini kuweni ni wenye kusimamia ushahidi kwa ajili ya Allah kwa uadilifu na wala kusiwapelekeeni kuwachukia watu kutofanya uadilifu fanyeni uadilifu huko ndiko kundiko kuliko karibu zaidi na ucha Mungu…’’. Al maidah 8.

Kitabu hicho kimekosa sifa zote za kitaalamu kuazia uadilifu, ukweli, uhakika wa tafiti za kielimu,bali kimegubikwa na chuki, dhulma, uongo,na ujahili katika mambo ya kielimu.

Unapotaka kuuzungumzia upotovu wa mtu au watu au madhehebu yoyote ile basi insafu ni kuyanukuu yale yao wanayoitakidi kutoka kwenye vitabu vyao vya rejea na si kunukuu itikadi zao kutoka kwa maadui zao na kama hutofanya hivyo na likiwa lengo lako ni kuufikia ukweli basi basi ujue kwamba hutoupata.

Na hili ndilo alilolifanya Khalifa Khamis mas’ala yote ya itikadi yanayo muhusu sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahab ameyanukuu kutoka kwa kina al Nab’hany,Dah’laany,mr Humphrey n.k.

Je sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahab hakuandika vitabu?
Je vitabu vyake vinasema nini?
Je wanafunzi wake nao?

Je maulamaa wakubwa waliokuwa katika zama zake kama vile;

1-Imamu San'any mtunzi wa kitabu mashuhuri Subulus salaam.

2-Imamu Shawkaany mtunzi wa kitabu Naylul awtwaar na tafsiri maarufu kwa jina la Fat'hul Qadir.

3-Imamu mkubwa Iraq katika zama zake Abul Fadhli Sayyid Shukri al Aluusy.
4-Imamu wa Shamu katika wakati huo Ibn Bad'raan.

Na wengi wengineo,baada ya kubainikiwa na da'awa yake walisemaje?

Pia Khalifa angekuwa ana lengo la kujua ukweli na kuitafuta haki angeyapima yale yaliyomo katika vitabu vya sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahab kwa mizani ya Qur'an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia bila shaka haki ingembainikia mbele yake.

Lau kama Khalifa angetaka kuufikia ukweli angezilinganisha kauli za sheikh Muhammad Ibn Abdul Wahab na kauli za maulamaa wakubwa wa ahli sunna wal jamaa waliomtangulia kabla yake kwa karne nyingi.

Lau kama Khalifa angetaka kuujua ukweli angezifanyia utafiti wa kielimu haduthi anazozitumia na kuangalia kauli za maulamaa wakubwa wa hadithi zinasemaje?

Lau kama Khalifa angekuwa anakusudia kuineza haki basi angerejea tafsiri za maneno kama vile neon 'najdi' ni nini makusudio yake katika kauli ya bwana mtume -swallallaahu alayhi wasallam- na anasemaje Imamu al khattaby na al Hafidh Ibn Hajar al Asqalaany kuhusu neno hilo? Na bwana mtume swallallaahu alayhi wasallam alikusudia wapi alipoitaja Naj'di?

Lakini yote hayo ameyafumbia macho kwa makusudi kwa lengo la kutaka

kuipotosha haki akidhani kwamba Allah hatowafichua waongo akidhani kwamba Allah atakuwa ni mwenye kughafilika na wayatendayo madhalimu !

"ولا تحسبنّ الله غافلا عما يعمل الظالمون ".

‘‘Na wala usidhani yakwamba Allah ni mwenye kughafilika kwa yale wanayoyatenda madhalimu..’’.

NI NANI SHEIKH MUHAMMAD IBN ABDIL WAHAB?

1-Jina lake na nasabu yake;
Yeye ni Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahab Ibn Sulaymaan Ibn Aly Ibn Muhammad al Tamimiy.

2-Mwaka na mahali alipozaliwa
Sheikh Muhammad amezaliwa mwaka 1115 H (1703 M)na kufariki mwaka 1206 H(1794 M) ameishi miaka 91 takriban,na amezaliwa katika kitongoji cha Uyaina mashariki mwa nchi ya Saudi Arabia.

3-Masheikh zake waliomsomesha;

Sheikh Muhammad -Allah amrehemu- ameichukua elimu yake ya awali kutoka kwa baba yake mzazi sheikh Abdul Wahab Ibn Sulaymaan ambaye alikuwa ni kadhi katika eneo hilo la Uyaina na ni mwanawachuoni katika madhehebu ya kihambali.
Sheikh Muhammad -Allah amrehemu- alisoma kwa baba yake fiqhi ya kihambali na akakihifadhi kitabu cha Allah (Qur’an) na hali yakuwa umri wake hauja petuka miaka 10.
-Pia amesoma kwa sheikh Abdallah Ibn Ibrahim al madany.
-Sheikh Muhammad Hayaat Sindiy mwanawachuoni wa elimu za Hadithi katika miji mitakatifu ya Makka na Madina.
-Sheikh Muhammad al Maj’mui’y.
-Sheikh Aly Afandiy al Daaghistaniy.
-Sheikh Abdallah Salim al Basriy.

-Na sheikh Sib'ghatallaahi al Haydariy.

Wanafunzi wa sheikh Muhammad;
1-Su'ud Ibn Abdil Aziz Ibn Muhammad Ibn Su'ud.
2-Mtoto wake; Husein Ibn Muhammad.
3-Mtoto wake ;Aly Ibn Muhammad.
4-Mtoto wake; Abdullahi Ibn Muhammad.
5-Mjukuu wake;Abdul rah'man Ibn Husein Ibn Muhammad.
6-Sheikh al allaamah Hamad Ibn Naasir Ibn Uth'maan Ibn Ma'mar.
7-sheikh al allaama Husein Ibn Ghannaam.
Na wengineo wengi.

Vitabu alivyoandika;

1-Kitaabu Tawhiid.
2-Kitaabul Imani.
3-Usuulul Imani.
4-Fadhailul Islami
5-Fadhailul Qur'an.
6-Kash'fus Shubuhaati.
7-Aadabul Mash'yi ilas Swalaat.
8-Masailul Jahiliyyah.
9-Kitaabul Kabair.
10-Mukh'tasarul Shar'hil Kabiri wal Insaaf.
n.k.

madhehebu yake;
Sheikh Muhammad Ibn Abdul wahab alikuwa ni mfuasi wa madhehebu ya Hambali moja kati ya madhehebu nne za ki fiq'hi za Ah'li Sunna wal Jamaa. Na katika mambo ya kiitikadi alikuwa na itikadi ya Imamu Ah'mad Ibn Hambali mmoja kati ya maulamaa madhehebu nne.

Amesema Imamu shihaabu din al Alousiy;

وقال العلامة الآلوسي رحمه الله فى كتابه تاريخ نجد ص 51-53:

"والحاصل أن مذهبهم فى أصول الدين مذهب أهل السنة والجماعة وأن طريقتهم طريقة السلف التي هي الطريق الأسلم بل الأحكم ...

وأنهم فى الفروع على مذهب الإمام أحمد بن حنبل نضّرالله وجهه ولا ينكرون على من قلّد أحدا من الأئمة الأربعة دون غيرهم...

وأما ما يكذب عليهم سترا للحق وتلبيسا على الخلق بأنهم يفسرون القرآن برأيهم ويأخذون من الحديث ما وافق فهمهم من دون مراجعة شرح ولا معول على شيخ وأنهم يضعون من رتبة النبي صلى الله عليه وسلم وأنه ليس له شفاعة...

وينهون عن الصلاة عليه وأنهم يكفّرون الناس إلى غير ذلك من الإفترآت فكل ذلك زور عليهم وبهتان وكذب محض من خصومهم أهل البدع والضلال.

بل أقوالهم وأفعالهم وكتبهم على خلاف ذلك كله فمن روى عنهم شيئا من ذلك أو نسبه إليهم فقد كذب عليهم وافترى..."

## دفاع العلماء عن الشيخ ودعوته

**ألف علامة العراق فى وقته أبو المعالي محمود شكري الآلوسي 1342هـ كتابا سماه غاية الأماني فى الرد على النبهاني (يوسف بن إسماعيل بن يوسف النبهاني 1350هـ)**

**قال الشيخ محمد رشيد الرضا فى تقريظه لهذا الكتاب:**

**"كتاب مؤلف من سفرين كبيرين لأحد علماء العراق المكنى لأبي المعالي الحسيني السلامي الشافعي رد فيهما ما جاء به النبهاني فى كتابه شواهد الحق من الجهالات والنقول الكاذبة والآراء الساخفة والدلائل المقلوبة فى جواز الإستغاثة بغيرالله وما تعدى به طوره من سب أئمة العلم وأنصار السنة كشيخ الإسلام ابن تيمية...".**

**مجلة المنار مجلد 12/ص 785.**

**وقال العلامة الآلوسي رحمه الله فى كتابه تاريخ نجد ص 51-53:**

**"والحاصل أن مذهبهم فى أصول الدين مذهب أهل السنة والجماعة وأن طريقتهم طريقة السلف التي هي الطريق الأسلم بل الأحكم ...**

**وأنهم فى الفروع على مذهب الإمام أحمد بن حنبل نضّرالله وجهه ولا ينكرون على من قلّد أحدا من الأئمة الأربعة دون غيرهم...**

**وأما ما يكذب عليهم سترا للحق وتلبيسا على الخلق بأنهم يفسرون القرآن برأيهم ويأخذون من الحديث ما وافق فهمهم من دون مراجعة شرح ولا معول على شيخ وأنهم يضعون من رتبة النبي صلى الله عليه وسلم وأنه ليس له شفاعة...**

وينهون عن الصلاة عليه وأنهم يكفّرون الناس إلى غير ذلك من الإفترآت فكل ذلك زور عليهم وبهتان وكذب محض من خصومهم أهل البدع والضلال.

بل أقوالهم وأفعالهم وكتبهم على خلاف ذلك كله فمن روى عنهم شيئا من ذلك أو نسبه إليهم فقد كذب عليهم وافترى...".

وقال رحمه الله فى ص 56:
"وغالب من أشاع ذلك هم أهل البدع والأهواء الذين اتخذوا دينهم لهواً ولعباً وكذبوا بأقوالهم وأفعالهم على الدين المبين الذي هو بعيد عنهم بمراحل وهم الدجالون الجالبون على الإسلام كل عار وإلا فأهل الإيمان هم الذين يستمعون القول فيتبعون أحسنه".

قال الإمام الشوكاني رحمه الله تعالى فى كتابه البدر الطالع 357/1:
"فإن صاحب نجد وجميع أتباعه يعملون بما تعلموه من محمد بن عبدالوهاب وكان حنبليا ثم طلب الحديث بالمدينة المشرفة فعاد إلى نجد وصار يعمل باجتهادات جماعة من متأخري الحنابلة كابن تيمية وابن القيم وأضرابهما....
وقد كاتبه وسأله بيان ما يعتقده فرأيت جوابه مشتملا على اعتقاد حسن موافق للكتاب والسنة فالله أعلم بحقيقة الحال".

وقال الإمام الشوكاني أيضا فى كتابه 357/1:
"ومن جملة ما يبلغنا عن صاحب نجد أنه يستحل سفك دم من لم يحضر الصلاة فى جماعة وهذا إن صح غير مناسب لقانون الشرع...
وتبلغ أمور غير هذه الله أعلم بصحته وبعض الناس يزعم أنه يعتقد اعتقاد الخوارج وما أظن ذلك صحيحا".

ويقول الإمام الشوكاني رحمه الله وهو يثني على كتب الشيخ محمد بن عبدالوهاب:
"وفى سنة 1215 وصل من صاحب نجد المذكورمجلدان لطيفان أرسل بهما إلى حضرة مولانا الإمام حفظه الله
أحدهما يشتمل على رسائل لمحمد بن عبدالوهاب كلها فى الإرشاد إلى إخلاص التوحيد والتنفير من الشرك الذي يفعله المعتقدون فى القبور وهي رسائل جيدة مشحونة بأدلة الكتاب والسنة.
والمجلد الآخر يتضمن الرد على جماعة من المعاصرين من فقهاء صنعاء وصعدة ذاكروه فى مسائل متعلقة بأصول الدين وبجماعة من الصحابة فأجاب عليهم جوابات محررة مقررة محققة تدل على أن المجيب من العلماء المحققين العارفين الكتاب والسنة".
انظر الكتاب البدر الطالع 357/1.
قال الإمام السيد محمود شكري الآلوسي رحمه الله:
"وخصومهم يسمون أتباعه "الوهابية" وهذه النسبة ليست بصحيحة والسنة فى الحقيقة إنما هي

**إلى الشيخ محمد لأنه هو الذي دعا الناس إلى ترك ما كانوا عليه من البدع والأهواء ونصر السنة وأمر باتباعها وقد خالف أباه فيما كان عليه...".**
**انظر تاريخ نجد ص 113**